

Jibu: Tusome,

Waamuzi 18:2 “Basi wana wa Dani wakatuma watu wa jamaa zao, watu watano katika hesabu yao yote, watu mashujaa, kutoka Sora, na kutoka Eshtaoli, ili kuipeleleza hiyo nchi, KUIAUA; wakawaambia, Haya, endeni mkaikague nchi hii; basi wakaifikilia nchi ya vilima vilima ya Efraimu, hata nyumba ya huyo Mika, Wakalala huko”

Kuiaua nchi maana yake ni **KUITEMBELEA NCHI au KUIZURU**. Kwahiyo watu wanaozunguka zunguka ndani ya nchi kwa lengo la kuipeleleza au kwa lengo la utalii, maana yake ni **WAMEIAUA HIYO NCHI**.

Mungu wetu anaiua dunia hii tunayoishi, kutafuta watu wanaomcha yeye, kuwatia nguvu na kuonyesha uweza wake juu yao.

2Nyakati 16:9 “Kwa maana macho ya Bwana hukimbia-kimbia duniani mwote, ili ajionyeshe mwenye nguvu kwa ajili ya hao, waliokamilika moyo kuelekea kwake...”

Lakini pia adui yetu shetani **ANAIUA** dunia nzima kutafuta mwenye haki mmoja amwangushe..

Ayubu 1:6 "Ilikuwa, siku moja ambayo hao wana wa Mungu walikwenda kujihudhurisha mbele za Bwana, Shetani naye akaenda kati yao.

7 Bwana akamwuliza Shetani, Umetoka wapi wewe? Ndipo Shetani akamjibu Bwana, na kusema, Natoka katika kuzunguka-zunguka duniani, na katika kutembea huku na huku humo.

8 Kisha Bwana akamwuliza Shetani, Je! Umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na mwelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu"

Hivyo hatuna budi kuutunza ukamilifu wetu ili tusije tukanaswa katika mitego ya shetani na hatimaye kuanguka kabisa.

Maran atha!

Tafadhali shea na wengine ujumbe huu;

Pia Kwa maombezi/ Ushauri/ Maswali/ Whatsapp:

Tuandikie katika BOXI la Maoni hapo chini au

Piga namba hizi: +255693036618 au +255789001312

Mada Nyinginezo:

Biblia inaposema “Wote tumetenda dhambi” si inamaanisha hakuna mtakatifu duniani?

TABIA ZITAKAZOMTAMBULISHA MPINGA-KRISTO AJAYE.

Marago ni nini? (Waamuzi 10:18)

KWANINI DANI ALIKAA KATIKA MERIKEBU.

MUNGU HANA MBARAKA MMOJA TU!..MWAMINI.

Rudi nyumbani

Share on:

WhatsApp

Kuiaua Nchi ni kufanya nini? (Waamuzi 18:2).

[Print this post](#)